

## MKATABA WA KUPANGISHA ENEO LA BIASHARA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 04 Mwezi wa February Mwaka 2022.

### **BAINA YA**

Ndugu **ELISABAOT MARUNDA KIMAMBO** wa sanduku la Posta 9560 MOSHI (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "**Mwenye eneo**" kwa upande mmoja.

### **NA**

**JEA STEEL COMPANY LIMITED** Kampuni ilisajiliwa kwa mujibu wa sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "**MPANGAJI**" kwa upande wa pili.

**KWA KUWA MPANGISHAJI** ni mmiliki halali wa eneo lililopo kitongoji cha Teua Juu, kijiji cha Koresa, kata ya Kirua Vunjo kusini wilaya ya Moshi Vijijini Lenye upana wa mita 70 na uyrefu wa mita 70 na ameamua kumpangishia mpangaji na mpangaji amekubali kupanga eneo hilo kwa ajili ya biashara .

### **HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA HAYA YAFUATAYO:-**

- 1. KWAMBA**, pande zote mbili zimekubaliana kuwa mpangishaji atampangishia mpangaji tajwa hapo juu kwa makubaliano kuwa mpangaji atajenga kiwanda cha kutengeneza mabati kwenye eneo tajwa hapo juu kwa gharama zake.
- 2. KWAMBA**, Mpangaji atamlipa mpangishaji / mwenye eneo kiasi cha shilingi za kitanzania laki tano tu ( Tsh 500,000/=) kwa mwezi kwa muda wa miaka kumi ili kufidia ujenzi wa kiwandacha mabati kilichojengwa na mpangaji na baada ya hapo pande zote mbili zinawezakuingia makubaliano mapya,
- 3. KWAMBA**, Malipo yote yatafanyika kupitia akaunti ya Mpangishaji ya EXIM BANK katika akaunti Na. **5774545557**
- 4. KWAMBA**, mkataba huu utanza rasmi tarehe 01/12/2024 hii ni baada ya ujenzi wa kiwanda kukamilika pamoja na mashine na kuisha tarehe 02/01/2034 na unaweza kurejewa upya kulingana na makubaliano mapya.
- 5. KWAMBA**, ni jukumu la Mpangaji kulipia umeme na maji katika eneo alilopanga kulingana na matumizi yake.
- 6. KWAMBA**, Mpangaji haruhusiwi kumrithisha mtu mwingine haki eneo mpangaji alilopanga ni kwa ajili ya biashara ya kutengeneza mabati tu.



05/03/2024

7. **KWAMBA**, Mpangaji atawajibika kuweka mazingira yake katika hali ya usafi kipindi chote cha mkataba na kuhakikisha kuwa kiwanda na eneo lote kwa ujumla linakuwa katika hali nzuri muda wote atakao kuwa kwenye mkataba.

8. **KWAMBA**, Mpangaji mara baada ya kipindi cha mkataba kuisha kama hakutoa taarifa ya kuendeleza upangaji wake kama ilivyoelezwa katika kifungu cha nne (4) hapa juu, itachukuliwa kuwa mpangaji hataki kuendeleza upangaji, hivyo mwenye eneo atakuwa huru kupangishia mtu mwingine.

9. **KWAMBA**, Baada ya mkataba kuisha mpangaji atawajibika kukabidhi vitu vyote vinavyoambatana na kiwanda kama vile funguo na kuhakikisha vitu vyote viko salama.

**MAKUBALIANO** haya yametiwa sahihi leo tarehe 04 mwezi February 2022 baada ya pande zote kuusoma na kuuelewa vizuri.

**KWA UPANDE WA MPANGISHAJI:**

**UMESAINIWA** na **KUTOLEWA** na  
**ELISABAOT MARUNDA KIMAMBO** ambaye  
Namfahamu binafsi/ametambulishwa na  
.....  
Leo hii tarehe 04 Mwezi February 2022.



**MPANGISHAJI**

**KWA UPANDE WA MPANGAJI:**

**UMESAINIWA** na **KUTOLEWA** na .....  
..... **kwa niaba ya JEA STEEL**  
**COMPANY LIMITED** .ambaye namfahamu  
binafsi/ametambulishwa na.....  
Leo hii tarehe 04 Mwezi February 2022



**MPANGAJI**

**MBELE YANGU.**

**JINA:** Estersia Linus Mrawa

**SAHIHI:** 

**ANUANI:** S.L.P 3041 moshi

**CHEO:** Wakili.

